East African Journal of Swahili Studies, Volume 7, Issue 1, 2024
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1803

East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 7, Issue 1, 2024
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Mikabala Tofauti ya Waandishi wa Vitabu vya Kiada kuhusu Kipengele cha Mtindo wa Uandishi Insha za Kiswahili Nchini Kenya

*Nester Ateya[1*], Eric Walela Wamalwa[1] na Stanley Adika Kevogo[2]*

[1] Chuo Kikuu cha Kibabii, S. L. P. 1699-50200 Bungoma, Kenya.
[2] Chuo Kikuu cha Jaramogi Oginga Odinga cha Sayansi na Teknolojia, S. L. P. 210-40601, Bondo, Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: ateyanester77@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1803**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*06 Machi 2024*

**Istilahi Muhimu**:

*Mikabala, Mtindo, Vitabu Vya Kiada, Ufundishaji, Ujifundishaji.*

**IKISIRI**

Makala haya yanabainisha mikabala ya waandishi wa vitabu vya kiada katika ufundishaji na ujifundishaji wa mtindo wa insha za Kiswahili kwa shule za upili nchini Kenya. Mikabala tofauti ya waandishi aghalabu huwa chanzo cha utata miongoni mwa walimu na wanafunzi na hivyo kuathiri matokeo ya mtihani wa kitaifa. Uchunguzi huu umekitwa kwa mihimili ya Nadharia ya Mtindo iliyoasisiwa na Louis Tonko Milic. Nadharia hii inashikilia kuwa mtindo hutegemea mtu binafsi. Utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo, mkabala wa kithamano. Idadi lengwa ya utafiti ni walimu wa somo la Kiswahili 73, wanafunzi 2,000 na vitabu vya kiada 7 vya shule za upili. Kwa hivyo, usampulishaji wa kimakusudi ulitumiwa kuteua walimu 22, wanafunzi 320 na vitabu vya kiada 6. Mbinu za ukusanyaji wa data zilizotumika ni uchanganuzi wa yaliyomo, mahojiano na hojaji. Data ilichanganuliwa kwa kutumia asilimia, majedwali na kuwasilishwa kiufafanuzi. Matokeo ya uchunguzi yanaonesha kwamba, matumizi ya vitabu vya kiada tofauti tofauti yanazua mikabala tofauti katika ufundishaji na ujifundishaji wa mtindo wa insha. Hali hii inatokana na waandishi wa vitabu kiada kuwa na mikabala tofauti kuhusu mtindo wa insha za Kiswahili. Matokeo ya uchunguzi huu ni muhimu kwa walimu na wanafunzi wa Kiswahili katika shule za upili, viwango vingine vya elimu na wakuza mitaala pamoja na waandishi wa vitabu vya kiada. Wizara ya Elimu pamoja na vyuo vya walimu kupitia warsha na maarifa zaidi ya yale ya vitabu vya kiada, watafaidi mikakati ya kuimarisha ufundishaji na ujifundishaji wa somo la insha.

**APA CITATION**

Ateya, N., Wamalwa, E. W. & Kevogo, S. A. (2024). Mikabala Tofauti ya Waandishi wa Vitabu vya Kiada kuhusu Kipengele cha Mtindo wa Uandishi Insha za Kiswahili Nchini Kenya. *East African Journal of Swahili Studies*, *7*(1), 114-123. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1803.

**CHICAGO CITATION**

Ateya, Nester, Eric Walela Wamalwa and Stanley Adika Kevogo. 2024. "Mikabala Tofauti ya Waandishi wa Vitabu vya Kiada kuhusu Kipengele cha Mtindo wa Uandishi Insha za Kiswahili Nchini Kenya". *East African Journal of Swahili Studies* 7 (1), 114-123. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1803.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1803

**HARVARD CITATION**

Ateya, N., Wamalwa, E. W. & Kevogo, S. A. (2024) "Mikabala Tofauti ya Waandishi wa Vitabu vya Kiada kuhusu Kipengele cha Mtindo wa Uandishi Insha za Kiswahili Nchini Kenya", *East African Journal of Swahili Studies*, 7(1), pp. 114-123. doi: 10.37284/jammk.7.1.1803.

**IEEE CITATION**

N. Ateya, E. W. Wamalwa & S. A. Kevogo "Mikabala Tofauti ya Waandishi wa Vitabu vya Kiada kuhusu Kipengele cha Mtindo wa Uandishi Insha za Kiswahili Nchini Kenya", *EAJSS*, vol. 7, no. 1, pp. 114-123, Mar. 2024.

**MLA CITATION**

Ateya, Nester, Eric Walela Wamalwa & Stanley Adika Kevogo. "Mikabala Tofauti ya Waandishi wa Vitabu vya Kiada kuhusu Kipengele cha Mtindo wa Uandishi Insha za Kiswahili Nchini Kenya". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 7, no. 1, Mar. 2024, pp. 114-123, doi:10.37284/jammk.7.1.1803.

## UTANGULIZI

Somo la uandishi wa insha katika lugha ya Kiswahili hufundishwa katika viwango mbalimbali nchini Kenya. Hufundishwa kama stadi mojawapo ya somo la Kiswahili na ambalo ni la lazima katika shule za msingi na upili. Kwa mujibu wa Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Kenya (TUMIKE) insha hufundishwa kama uandishi wa kiuamilifu na insha ya kawaida katika kiwango cha shule za upili (KIE, 2002). Kwa mujibu wa TUMIKE, wanafunzi katika kiwango cha shule ya upili wanapaswa kufundishwa aina zote za insha za kiuamilifu pamoja na zile za kawaida, sio tu kwa minajili ya mtihani bali kwa matumizi katika shughuli za maisha ya kila siku katika jamii baada ya shule. Kwa hivyo, makala haya yanabainisha mikabala tofauti ya waandishi wa vitabu vya kiada katika ufundishaji na ujifundishaji wa mtindo wa insha za Kiswahili katika shule za upili nchini Kenya.

Vitabu vya kiada ni nyenzo muhimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifundishaji wa insha katika shule za upili (Richards, 2001). Walimu na wanafunzi huvitegemea vitabu hivi katika maandalizi, ufundishaji na ujifundishaji wa somo la insha. Ufundishaji na ujifundishaji wa mtindo wa insha za Kiswahili ni muhimu na kwa hali hiyo ipo haja ya kuwepo ufafanuzi dhahiri na kuridhisha. Mtindo wa insha za Kiswahili umeibua mikabala tofauti miongoni mwa wataalamu na waandishi wa vitabu vya kiada katika shule za upili nchini. Hali hii inazua mtafaruku wa fafanuzi mbalimbali miongoni mwa wataalam na waandishi wa vitabu vya kiada. Ukosefu wa mwelekeo mmoja linganifu wa kufundishia mtindo wa insha ndiyo msukumo wa utafiti uliozalisha makala haya.

Mtindo ni namna ya kuandika insha. Insha inapotathminiwa kwa mujibu wa kigezo cha mtindo, vipengele kama vile unadhifu wa mtungo, hijai, mbinu mbalimbali za urutubishaji, uiakifishashaji, miongoni mwa vingine huzingatiwa (Nyariki, 2021; KNEC, 2020). Mtindo umefasiliwa kuwa ni sauti itokanayo na uchunguzi wa maneno yaliyoandikwa na kusemwa (Montin, 2011). Ni uteuzi na matumizi ya maneno mwafaka katika lugha inayohusika. Nyariki (2021) anaeleza mtindo kuwa ni namna ya kuandika insha huku Montin (2011) akisisitiza maneno yanayotumika katika uandishi wa insha.

Corbett (1998) anaainisha mbinu tatu za kufundishia mtindo wa uandishi ambazo ni uchambuzi, uigaji na uzalishaji. Mbinu yake uchambuzi wa mtindo wa nathari huwahitaji wanafunzi kuhesabu idadi ya sentensi katika insha na kuziainisha - sahili, ambatani, changamano, na kadhalika - kisha kuhesabu idadi ya maneno katika kila sentensi. Azma kuu ya zoezi hili ni kubaini usomekaji wa kipande cha andiko na kubainisha maeneo yanayoweza kusahihishwa na kuhaririwa (Butler, 2008). Katika kutumia mbinu ya uigizaji wanafunzi aghalabu huiga au hukariri mtindo waliotazama au kuusoma kwingineko. Kimsingi, wanafunzi huiga mitindo wa watunzi wengine; wanajumuisha miundo ya mitindo hiyo kwenye utunzi wao. Ujumuishaji wa aina hii baadaye hukuza ubunifu wao. Katika uzalishaji, wanafunzi wanahimizwa kutumia mfumo wa ukuzaji wa mitindo yao wenyewe. Mbinu hizi tatu hufanya kazi kwa imani kwamba mtindo ni sanaa inayoweza kufunzwa. Anashauri kuwa,

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1803

wanafunzi watumie mitindo ya uandishi wa insha iliopo katika lugha lakini wawe makini kujifunza mitindo mipya inayozuka na ikiwezekana washiriki katika kubuni mitindo mipya. Anaunga mkono mikabala tofauti ya mtindo wa uandishi wa insha.

Utafiti uliozalisha makala haya ulidhamiria kuchunguza mikabala tofauti ya waandishi wa vitabu vya kiada ili kubaini athari zake katika ufundishaji na ujifundishaji wa mtindo wa insha za Kiswahili. Ili kubaini mikabala ya waandishi tofauti wa vitabu vya kiada katika ufundishaji na ujifundishaji wa insha katika hali halisi, uchunguzi wenyewe ulifanywa katika eneo la kaunti ndogo ya Mumias Magharibi, Kaunti ya Kakamega. Maswali yaliyoongoza uchunguzi ni: Je, waandishi wa vitabu vya kiada wana maelezo sawa kuhusu mtindo wa insha? Je, kitabu kimoja kinafaa kwenye michakato ya maandalizi na ufundishaji wa mtindo? Je, vitabu vya kiada tofauti huzingatia urefu wa insha inayohusika? Kimsingi, majibu ya maswali haya ndiyo kichocheo cha uchunguzi unaoripotiwa katika makala haya. Makala yenyewe yanawasilishwa katika sehemu kuu tano. Sehemu ya kwanza ya utangulizi unaofafanua usuli wa utafiti. Inafuatiwa na mbinu za utafiti, misingi ya nadharia na kisha uchanganuzi mjadala kuhusu mikabala mbalimbali ya waandishi wa vitabu vya kiada kuhusu mtindo wa insha za KiswahiIi. Hatimaye, hitimisho limewasilishwa.

## MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ulitumia mkabala wa kithamano, muundo wa kimaelezo. Ulifanywa maktabani na nyanjani kwenye eneo la kaunti ndogo ya Mumias Magharibi, Kaunti ya Kakamega Magharibi mwa Kenya. Idadi lengwa ya utafiti ilihusisha vitabu vya kiada 6 kati ya 7 vya lugha ya Kiswahili. Jumla ya walimu 22 kati ya 73 wa Kiswahili na wanafunzi wa kidato cha 1-4, 320 kati ya 2,000 kutoka kaunti ndogo ya Mumias Magharibi walishiriki katika uchunguzi huu. Walimu waliteuliwa kimaksudi kwa kuzingatia vigezo vya tajriba ya kazi na viwango vya elimu. Wanafunzi walichaguliwa kwa kutegemea idadi ya madarasa katika kila kidato na jinsia.

Vitabu vya kiada vilivyoidhinishwa na TUMIKE, kwa kurejelea kidato, idadi na aina za insha. Insha za wanafunzi 40 pia zilichaguliwa kimakusudi kutoka kwa madaftari ya wanafunzi wa kidato cha 1-4 kwa kuzingatia uwezo wa wanafunzi kielimu. Utafiti wetu ulirejelea vitabu vya kiada 7 katika kubaini mikabala ya matumizi ya vitabu vya kiada tofauti katika ufundishaji na ujifundishaji wa mtindo wa insha za Kiswahili. Vitabu hivi viliteuliwa kwa kudhamiria kwa sababu vinatumika katika shule za upili nchini Kenya. Vitabu vyenyewe vimeorodheshwa katika jedwali Na. 1 lifuatalo:

**Jedwali 1: Orodha ya vitabu ya kiada**

| Shirika la Uchapishaji | Anwani |
|---|---|
| Longhorn Kenya | *Chemichemi za Kiswahili* |
| Oxford University Press | *Kiswahili Fasaha* |
| East Africa Educational Publishers | *Johari ya Kiswahili* |
| Keya Literature Bureau | *Kiswahili kwa kidato* |
| Longman Kenya | *Hazina ya Kiswahili* |
| Moran Publishers | *Uhondo wa Kiswahili* |
| Phoenix Publishers | *Darubini ya Kiswahili* |

Mbinu za ukusanyaji data zilizotumiwa ni uchanganuzi wa yaliyomo, hojaji na mahojiano. Kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi wa yaliyomo, matini ya waandishi tofauti wa vitabu vya kiada yalichambuliwa katika muktadha wa ufundishaji na ujifundishaji wa insha za Kiswahili. Yaliyomo katika insha teule za wanafunzi pia yalichanganuliwa. Isitoshe, kwa kutumia mbinu za hojaji na mahojiano maoni ya walimu na wanafunzi yalikusanywa kuhusu mikabala inayoibuliwa na matumizi ya vitabu vya kiada tofauti katika ufundishaji na ujifundishaji

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1803

wa mtindo wa insha. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa kutumia asilimia, majedwali na kuwasilishwa kimaelezo.

## MSINGI WA NADHARIA

Makala hii iliongozwa na Nadharia ya Mtindo (NYM). Nadharia hii iliasisiwa na Louis Tonko Milic mnamo mwaka wa 1965. Nadharia hii inashikilia kuwa mtindo hufafanuliwa kwa mujibu wa athari zake kwa msomaji, chanzo cha maarifa au akili, kwa sababu mtindo ni kipawa cha kuzaliwa cha kiisimu, ubunifu na maadili ya lugha inayohusika.

Nadharia ya Mtindo ina mihimili mitatu. Mhimili wa kwanza ni ubinafsi. Mhimili huu unashikilia kwamba, mtindo hutegemea mtu binafsi. Ubinafsi wake hudhihirika kupitia jinsi anavyojieleza na kucheza densi. Mtu huandika kulingana na maumbile yake. Mtindo wake wa uandishi huwasilisha tabia yake inayodhihirika kupitia hati na shughuli zake zote. Kwa hivyo mtindo hauwezi kuteuliwa kwa hiari bali mhusika huzaliwa nao. Mhimili huu humpa mwalimu na mwanafunzi mtindo mmoja pekee wa kuwasilisha ujumbe.

Mhimili wa pili ni muundo au uwili. Mtu hubuni mawazo bila mpangilio na huweza kuyawasilisha kutegemea tukio au muktadha baada ya kuchumbua miundo tofauti. Mhimili huu humpa mwalimu nafasi ya kukuza njia mbadala au zaidi ya moja ya kuwasilisha ujumbe. Milic (1965) anaeleza kuwa, mtindo ni sawa na mavazi, mtu huweza kuvalishwa mavazi tofauti kulingana na tukio.

Hatimaye, mhimili wa tatu unahusu mada na mtindo. Kwa mujibu wa mhimili huu, hakuna tofauti kati ya mada na mtindo.

Katika makala haya, mhimili wa kwanza na wa pili ulitumika katika uchanganuzi wa matini ya waandishi tofauti wa vitabu vya kiada ili kudhihirisha namna wanavyojenga mtungo wa insha kwa kuzingatia mtindo wa uandishi wa insha. Mihimili hii ilisaidia kulishughulikia madhumuni ya utafiti. Sehemu ifuatayo inajadili na kuwasilisha matokeo ya utafiti.

## MIKABALA TOFAUTI KUHUSU MTINDO WA INSHA ZA KISWAHILI

Sehemu hii inachambua na kujadili mikabala tofauti ya waandishi wa vitabu vya kiada kwa kurejelea insha za mjadala, resipe, ratiba na mahojiano. Mikabala ya wanafunzi na walimu kuhusu mtindo wa insha pia imewasilishwa.

### Mikabala ya Uandishi wa Insha Vitabuni

Mikabala tofauti ya baadhi ya waandishi wa vitabu vya kiada kuhusu insha za Kiswahili ilichunguzwa. Vitabu vya kiada mbalimbali vilichambuliwa (Rejelea Jedwali Na. 1) kwa madhumuni ya kubainisha mikabala iliyotumika. Uchambuzi wenyewe ulirejelea insha za mjadala, resipe, ratiba na mahojiano katika vitabu vya kiada vinavyolengwa wanafunzi wa kidato cha 1-4. Mikabala ya tofauti ya waandishi ilichambuliwa kwa mujibu wa anwani, utangulizi, yaliyomo na hitimisho.

### Uandishi wa Mjadala

Vonyoli & wenzie (2015) *Kiswahili Kitukuzw*e wanaeleza kuwa, kuna mikabala miwili ya kuandika insha ya mjadala ambapo mwandishi hueleza kwa uwazi na mapana kuhusu suala fulani hadi akahitimisha. Kwa mfano, ‘Jadili umuhimu wa simu tamba katika jamii ya leo.’ Hapa, mwandishi anahitajika kutoa hoja za kudhihirisha umuhimu wa simu tamba. Pili, mjadala ambapo mwandishi anapaswa kutoa hoja za pande zote mbili za suala linalohusika kisha, katika aya ya mwisho atoe uamuzi au maoni yake. Ilibainika kwamba, mjadala huu unaweza kutekelezwa kwa njia mbili. Mwandishi aeleze upande mmoja kwanza, kama vile kuunga mkono kisha kupinga mjadala na hatimaye atoe uamuzi. Mwandishi anatakiwa aeleze jinsi upande mmoja ni bora kuliko mwingine na mwishowe atoe maoni yake. Hata hivyo, waandishi hawa hawajatoa kielelezo cha mfano wa insha ya mjadala.

Ngure & wenzie (2011) katika *Hazina za Kiswahili* wanasema kuwa, insha ya mjadala huwasilisha misimamo inayopingana kuhusu wazo au anwani iliyotolewa. Kuna hoja za kuunga mkono na zile za kulipinga wazo hilo. Wanaeleza

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1803

kuwa, katika umbo la insha ya mjadala, mwandishi huandika hoja akijadili moja baada ya nyingine huku akiwasilisha misimamo ya pande zote mbili kwa kila hoja. Kila aya hushughulikia hoja moja tu. Hoja hufafanuliwa kwa utaratibu, huku ikizua pinzani, kisha hoja pinzani inafafanuliwa. Hatimaye, uamuzi hutolewa kukamilisha aya. Katika aya ya mwisho ambayo ni tamati mwa insha, msimamo hutolewa kutegemea upande uliopewa uzito. Ngure & wenzie (2011) wametoa kielelezo cha mfano wa insha ya mjadala. Anwani ya insha haidhihirishi kuwa insha ni ya mjadala na imeandikwa kwa herufi ndogo, "ukoloni barani afrika (uk.34 )". Pili, mtindo wa kuandika yaliyomo ni tofauti kabisa na kinyume cha maelezo yao. Wametoa hoja za kupinga kisha hoja za kuunga mkono. Matokeo yamewasilishwa katika Jedwali Na. 2 lifuatalo:

**Jedwali 2: Mikabala kuhusu mtindo wa mjadala**

| Mikabala ya Uandishi | Vitabu | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| Kuunga mkono pekee | 1 | 33.33% |
| Kupinga tangu mwanzo hadi mwisho | 1 | 33.33% |
| Kuunga mkono, kupinga kisha kutoa msimamo | 1 | 33.33% |

**Chanzo:** Data Nyanjani (2022)

Kutokana na jedwali hili, vitabu vitatu vya kiada vilivyorejelewa vilidhihirisha mikabala tofauti ya uandishi wa insha ya mjadala. Ilibainika kuwa uandishi wa insha ya mjadala umezua mikabala mitatu miongoni mwa waandishi. Kwanza, kuunga mkono, kupinga na mwisho kuunga na kupinga kwa wakati mmoja.

**Uandishi wa Resipe**

Vonyoli & wenzie (2007) hawajafafanua maana ya resipe wala maelezo ya mtindo na utaratibu wa kuandika insha hii. Lakini wametoa vielelezo vya mfano vya insha ya resipe. Mifano hiyo ina anwani ambayo imetaja aina ya chakula na idadi ya walaji bila kuonesha ni resipe. Isitoshe, anwani imeandikwa kwa herufi ndogo. Kuna viambata na utaratibu wa kupika chakula kichohusika. Mwisho, wameeleza maandalizi mezani na vyakula vingine vya kuliwa pamoja na kitoweo kinachohusika. Kwa upande mwingine, Ngure & wenzie (2004) wanaeleza kuwa, resipe ni maelezo ya kutayarisha chakula fulani. Hurejelea vitu vitakavyotumiwa, vipimo na namna ya kukipika chakula. Kipimo cha joto na mada utakaotumiwa na kutaja idadi ya walaji. Wametoa kielelezo cha mfano cha resipe ambapo anwani imeandikwa kwa herufi ndogo na haina idadi ya walaji. Kuna viungo na utaratibu wa maandalizi umeelezwa kwa sentensi moja kila hatua.

Mumbo & Ngamia (2013) katika *Johari ya Kiswahili* wanafafanua resipe kuwa ni maelezo ya upishi. Maelezo yametolewa kwa lugha ya shuruti na msamiati unahusu upishi. Kiasi cha viungo na chakula huweza kukadiriwa kutegemea walaji. Muda na njia za upishi hubainishwa. Wametoa kielelezo cha mfano wa resipe unaohusisha pia michoro. Mfano hauna anwani, viungo na kiasi kimetajwa kisha utaratibu umeelezwa kwa sentensi moja kila hatua.

Aidha, Wamitila (2012) katika *Chemichemi za Kiswahili* anaeleza kuwa resipe ni neno linalotumiwa kuelezea mwongozo wa mapishi, yaani maelekezo ya jinsi ya kutayarisha mapishi fulani, nini kinachohitajika na hatua za kuandaa chakula hicho. Anaelezea kuwa resipe ina sehemu tatu kuu: anwani ( jina la chakula kinachoandaliwa), mahitaji ya kuandaa chakula hicho na hatua za mapishi. Ametoa mifano miwili ya resipe, mmoja wa chakula kinachohitaji viungo na muda mfupi kuandaa na mfano wa pili wa chakula kinachohitaji viungo tofauti na muda mrefu kuandaa. Katika mfano wa kwanza maandalizi yameelezwa kwa hatua ya sentensi moja ilhali mfano wa pili wenye viungo vingi, hatua zimefafanuliwa katika aya moja kila hatua na msamiati wa upishi umezingatiwa.

Kwa ujumla, imebaini kuwa insha ya resipe ina mikabala minne. Kipimo cha joto, muda wa

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1803

maandalizi, urefu wa insha na njia mbadala ya kuandika insha hii. Matokeo yamesilishwa kwa muhtasari katika Jedwali Na. 3 lifuatalo:

**Jedwali 3: Mikabala kuhusu mtindo wa resipe**

| Mikabala ya Uandishi | Vitabu | Asilimia |
|---|---|---|
| Kipimo cha joto na muda wa kutayarisha chakula | 2 | 50% |
| Hatua za maandalizi katika sentensi fupifupi | 2 | 50% |
| Hatua za maandalizi katika aya | 2 | 50% |
| Njia mbadala ya kuandaa chakula | 2 | 50% |

**Chanzo:** Data Nyanjani (2022)

Jedwali hili linaonesha matokeo ya uchanganuzi wa vitabu vinne. Vitabu viwili vilidhihirisha mikabala linganifu katika kila mojawapo ya mikabala minne tofauti iliyorejelewa kuhusu uandishi wa resipe.

**Uandishi wa Ratiba**

Walibora & Wangendo (2004) *Uhondo wa Kiswahili* wanaeleza kuwa, ratiba ni mfululizo au mfuatanisho wa hatua zitakazofuatwa katika shughuli fulani kulingana na muda uliokubaliwa. Wanaeleza kuwa ratiba huwa na shughuli na wakati zitakapofanyika na wapi. Kitendo kitaanza na kuisha saa ngapi. Wanasisitiza kwamba kitendo kiambatanishwe na wakati kitakapotendeka, kisha mapokezi rasmi mwanzo na mwishoni. Wametoa mfano wa ratiba ambao una anwani. Anwani hii imeanza kwa neno ratiba, shughuli, mahali pa tukio na tarehe. Anwani imeandikwa kwa herufi ndogo na wakati wa shughuli umeandikwa kwa tarakimu na majira hayajaelezwa. Shughuli imefafanuliwa kwa sentensi moja fupi.

Ratiba ni mpangilio wa matendo au matukio yanayotarajiwa kutendeka na hupangwa kufuatiana na kutekeleza kwayo; ambacho hutaja shughuli husika, mahali na tarehe (Vonyoli & wenzie, 2015). Wakati wa kutendeka kwa matukio huonyeshwa. Anwani inafaa iandikwe kwa herufi kubwa. Saa au wakati huendelezwa kimataifa kwa kutumia tarakimu kisha majira kwa mfano, saa 4:30 alfajiri. Wameonesha tukio linaanza saa ngapi hadi wakati litaisha (8:00-10:00 asubuhi). Wametoa kielelezo cha mfano wa ratiba ambapo shughuli imeelezwa kwa undani katika aya moja.

Ratiba ni mpangilio wa mfulilizo wa mambo yanayofanyika katika shughuli kulingana na wakati uliotengwa (Wamitila & Waihiga, 2010). Kichwa huwa na shughuli husika, tarehe na mahali pa shughuli. Tukio liambatishwe na wakati wa kutendeka kwake. Waandishi hawa wametoa mfano wa ratiba ambao kichwa chake kimeandikwa kwa herufi ndogo. Yaliyomo yameelezwa kwa sentensi moja huku wakati ukiandikwa kwa nambari bila majira. Muhtasari wa matokeo haya umewasilishwa katika Jedwali Na. 4 lifuatalo:

**Jedwali 4: Mikabala kuhusu mtindo wa ratiba**

| Mikabala ya Uandishi | Vitabu | Asilimia |
|---|---|---|
| Kuandika saa kwa kutumia nambari | 3 | 100% |
| Kuandika majira au wakati wa siku | 1 | 33.3% |

**Chanzo:** Data Nyanjani (2022)

Kwa mujibu wa Jedwali Na. 4 vitabu vinne vilirejelewa, vitatu vilikuwa na mikabala linganifu na kimoja kikiwa na mkabala tofauti. Ilibainika kwamba uandishi wa insha ya ratiba unazua mikabala minne tofauti kuhusu vipengele vya maana, anwani, majira na urefu wake. Waandishi tofauti wameibua mikabala tofauti kuvihusu vipengele hivi.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

**Uandishi wa Mahojiano**

Mahojiano au dayalojia ni mazungumzo ya watu wawili au zaidi ambapo wanafaidi suala fulani (Walibora &Wangendo, 2004). Wanaeleza kuwa mahojiano na dayalojia ni aina moja ya insha ambazo kwa kawaida huwa ni insha mbili tofauti. Wanasisitiza kuwa mwanafunzi ajihusishe kama mhusika katika insha hii. Waandishi hawa hawajatoa maelezo kuhusu mtindo wa insha hii.

Mahojiano ni hali ambayo mtu au watu wanaulizana maswali ili kutoa habari kuwahusu (Vonyoli & wenzie, 2015). Yupo mtu (mhojaji) anayeuliza maswali yanayohitaji majibu au maelezo kutoka kwa mhojiwa. Huwa na anwani inayoonesha mazungumzo ni kati ya akina nani. Pili, ni utangulizi unaoonesha muktadha na mahali walipo. Tatu, ni majina ya mhoji na mhojiwa yaandikwe upande wa kushoto yakifuatia na nukta pacha. Nne, mhoji aulize maswali ya kumchochea mhojiwa ili atoa majibu au maelezo yanayohitajika. Maswali hayana budi kuilenga mada inayohusika. Mhojiwa apewe nafasi ya kueleza mawazo hadi mwisho. Hata hivyo, waandishi hawa hawana kielelezo cha mfano wa mahojiano.

Wamitila & Waihiga (2010) wamerejelea mahojiano na dayalojia kwa pamoja licha ya kuwa aina mbili tofauti za insha. Wanatambua sifa zifuatazo za mahojiano. Kwanza, ni maelezo ya yanayofafanua ni nani anayefanya nini na wapi yakiwa yamefungiwa katika mabano. Majina ya wahusika yawe upande wa kushoto yakifuatiwa na nukta pacha. Mwandishi atumie alama za kuonesha hisia yawe na mtiririko wa mawazo. Isitoshe, waandishi hawa wametoa mfano wa mahojiano.

Ilibainika kwamba insha ya mahojiano imezua mikabala tofauti. Kwanza, mahojiano na dayalojia ni aina moja ya insha. Pili, mahojiano na dayalojia ni aina tofauti za insha lakini zifunzwe pamoja kwa sababu huchukua mtindo sawa. Tatu, ni iwapo mwandishi wa insha ya mahojiano na dayalojia anapaswa kujihusisha au la. Mwisho, ikiwa insha hizi zinapaswa kutoa maelezo ya muktadha wa mawasiliano.

**Mikabala ya Wanafunzi Kuhusu Mtindo**

Uchambuzi wa madaftari ya insha za wanafunzi ulitekelezwa ili kufahamu hali halisi ya ufundishaji na ujifundishaji wa mtindo wa insha darasani. Mwongozo wa uchanganuzi uliibua mikabala tofauti kuhusu sehemu za mtindo wa insha zifuatazo: anwani, utangulizi, yaliyomo, hitimisho pamoja na vigezo vya msamiati na sarufi.

**Anwani ya Insha**

Anwani ya insha ilizua mikabala tofauti. Kwanza, ni kuwepo au kutokuwepo kwa anwani na pili, ni ikiwa imeandikwa kwa herufi kubwa au ndogo. Asilimia 52% (wanafunzi 21) waliandika insha ikiwa na anwani. Kwa upande mwingine, asilimia 48% (wanafunzi 19) waliandika insha zao bila anwani. Ilibainika kuwa wanafunzi wengi walizingatia anwani katika insha za kiuamilifu na kuipuuza katika insha za kawaida kama vile mjadala, mdokezo na methali. Asilimia 85% (wanafunzi 34) waliandika anwani kwa herufi kubwa huku asilimia 15% (wanafunzi 6) wakizinakili kwa herufi ndogo. Hali hii ya kuandika anwani kwa herufi ndogo ni athari ya baadhi ya vitabu vya kiada ambavyo vimezingatia mtindo huo.

Wanafunzi wanaiga mtindo huu bila kufahamu kwamba, matumizi ya herufi kubwa na kuipigia mstari ni kuwezesha anwani ijitokeza bayana tofauti na sehemu zingine za insha. Waandishi wa vitabu vya kiada hufikia lengo hii kwa kutumia wino uliokolezwa katika uandishi wa anwani hata pale imeandikwa kwa herufi ndogo.

**Utangulizi wa Insha**

Matini za sehemu ya utangulizi wa insha za wanafunzi pia zilichunguzwa. Mikabala miwili ilijitokeza; kuwepo au kutokuwepo kwa utangulizi katika matini za insha. Asilimia 65% (wanafunzi 26) walizingatia sehamu ya utangulizi katika insha zao huku asilimia 35% (wanafunzi 14) wakiiwacha nje.

Sehemu hii ya insha inahitaji ubunifu wa hali ya juu kwa upande wa mwanafunzi. Uwezo ambao

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1803

hupatikana miongoni mwa mwanafunzi wenye uwezo wa juu na kadri wa kielimu na hukosekana miongoni mwa wale wenye uwezo wa chini wa kielimu. Wanafunzi wenye uwezo wa chini aghalabu hutatizwa na baadhi ya vitabu vya kiada ambavyo vimeipuuza sehemu hii. Kutokana na hali hii inashauriwa kwamba mwalimu na mwanafunzi wake wasisitize na kurejelea sehemu hii katika uandishi wa insha.

### Yaliyomo katika Insha

Yaliyomo ndiyo hubeba mada, kuwasilisha kiini au jumla ya ujumbe wa insha. Sehemu hii ilichanganuliwa katika viwango vinne: ukamilifu (maneno 375 na zaidi), robo tatu (maneno 275-374), nusu (maneno 175-274), na robo (kufikia maneno 174) (KNEC, 2020). Asilimia 17% (wanafunzi 7) walitumia urefu kamili, asilimia 25% (wanafunzi 10) robo tatu, asilimia 33% (wanafunzi 13) nusu na asilimia 25% (wanafunzi 10) robo. Matokeo haya yanawainisha wanafunzi kwa mujibu wa tofauti za uwezo wao kielimu. Iligundulika kwamba wanafunzi walishindwa kutimiza urefu unaohitajika wa baadhi ya tungo za insha za kiuaminifu. Pili, wanafunzi wengi waliiga mtindo wa lugha ya Kiingereza unaopendekeza ujumbe ufupishiwe kinyume na mahitaji ya mtihani wa insha za Kiswahili; hali iliyohusishwa na matokeo na uandishi duni.

### Hitimisho la Insha

Sehemu ya mwisho ni hitimisho la insha. Asilimia 44% (wanafunzi 17) waliizingatia sehemu hii huku asilimia 56% (wanafunzi 23) wakiipuuza au kuiacha nje. Kupitia kwa mbinu ya hojaji, mikabala ya wanafunzi pia ilijitokeza. Wasailiwa waliulizwa kuteua mbinu ambayo walimu wao huitumia kufundisha mtindo wa insha darasani. Walihitaji kuweka mkwaju kuteua miongoni mwa mbinu zifuatazo: maelezo darasani, kusoma vitabu, kuiga insha zingine, mtihani na marudio. Matokeo yalidhihirisha kuwa walimu wa Kiswahili hutumia mbinu tofauti kufunza mtindo wa insha darasani.

Aidha, wasailiwa waliombwa kuonesha vitabu vya kiada vinavyotumika darasani shuleni kwao kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne. Matokeo yalionesha kwamba, wasailiwa walitumia zaidi ya kitabu kimoja cha kiada kujifunza na kufunziwa mtindo wa insha. Vitabu vya kiada: *Kiswahili Kitukuzwe, Kiswahili Fasaha na Uhondo wa Kiswahili* viliongozwa kwa umaarufu kutokana na hali kwamba serikali ilivinunua na kuvisambaza katika shule zote za umma. Isitoshe, wasailiwa waliulizwa kuteua vitabu vya kiada walivyotumia darasani kujifunza mtindo wa insha. Asilimia 89% (wanafunzi 276) walichagua matumizi ya vitabu tofauti huku asilimia 11% (wanafunzi 34) walitumia kitabu kimoja.

### Mikabala ya Walimu Kuhusu Mtindo

Kupitia mbinu ya hojaji, walimu walihojiwa juu ya ulinganifu wa mkabala kuhusu maana na ufundishaji wa mtindo wa insha. Asilimia 31% (walimu 5) walikiri uwepo wa ufafanuzi sawa na maana ya mtindo na ufundishaji wake. Asilimia 69% (walimu 11) wateua uwepo wa ufafanuzi sawa wa maana ya mtindo na ufundishaji ambao ni tofauti. Ilibainika kuwa walimu walikuwa na ufafanuzi wa maana ya mtindo ulio sawa lakini wakatofautiana kuhusu jinsi walivyofunza mtindo darasani; hali inayoakisi uandishi wa vitabu vya kiada.

### Istilahi Zitumikazo Darasani Kufundishia Mtindo

Walimu waliulizwa kubainisha istilahi walizozitumia darasani kufundisha mtindo wa insha. Istilahi zifuatazo ziliorodheshwa: sura, muundo, mpangilio wa kazi, mtiririko wa mawazo, msamiati na mada. Ilidhihirika kuwa, wasailiwa wengi walitumia istilahi za sura, muundo pamoja na mtindo kufunza darasani. Asilimia 100% ya wasailiwa waliteua istilahi ‘sura’ kuwa ndiyo iliyotumiwa mara nyingi zaidi darasani. Matumizi ya istilahi hii ni ithibati ya uelewa wao wa mtindo. Muhutasari wa matokeo haya umewasilishwa katika Jedwali Na. 5 lifuatalo:

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1803

**Jedwali 5: Istilahi inayotumiwa na walimu kufunza mtindo**

| Istilahi Inayotumiwa | Mdafao |
|---|---|
| Sura | 16 |
| Muundo | 14 |
| Mpangilio | 13 |
| Mbinu | 6 |
| Mtiririko wa mawazo | 4 |
| Msamiati | 4 |
| Mada | 2 |

**Chanzo:** Data Nyanjani (2022)

Matokeo kwenye Jedwali Na. 5 hapo juu ni ithibati kwamba, maana na ufundishaji wa mtindo unaendelea kuwa mpana na kubadilika kuendana na mpito wa wakati; jambo linaloangazia hitaji la utafiti endelevu kuhusiana na mada hii. Uchunguzi wetu ulinuia kubaini jinsi mabadiliko ya aina hii yanavyojitokeza katika hali halisi za ufundishaji na ujifundishaji darasani.

### Usahihishaji wa Mtindo wa Insha

Walimu waliosailiwa waliulizwa kuhusu mambo waliyozingatia katika usahihishaji wao wa mtindo wa insha. Maoni waliyotoa yalionesha ulinganifu mkubwa. Asilimia 62% (walimu 10) walieleza kuwa walizingatia sura au muundo wa insha huku asilimia 38% (walimu 6) wakisema kuwa walitilia maanani vipengele vya sarufi, hijai na maudhui ya insha. Hali hii inadhihirisha kuwa walimu wana mikabala tofauti katika usahihishaji wao; asilimia 43% (walimu 7) walikiri kutoa maoni sawa, huku asilimia 57% (walimu 9) washikilia kuwa maoni ya walimu yalikuwa tofauti.

### Idadi ya Vitabu vya Kiada Vitumikavyo

Wasailiwa pia walihitajika kueleza ikiwa wanatumia kitabu kimoja cha kiada kuandaa nyenzo na makala ya kufundishia darasani. Asilimia 94% (walimu 15) walikiri kutumia vitabu vya kiada tofauti na mwalimu mmoja akitumia kitabu cha kiada kimoja pekee. Hata hivyo, ilibainika kwamba licha ya walimu kutumia vitabu vya kiada tofauti katika maaandalizi, waliwapa wanafunzi wao kitabu kimoja cha kiada kwa matumizi ya darasani. Matokeo haya yalidhihirisha kuwa walimu katika maandalizi yao huuzingatia mhimili wa pili wa Nadharia ya Mtindo. Mtindo na ufundishaji wake hubadilika kwa mujibu wa tukio na huwasilishwa kwa njia tofauti.

## HITIMISHO

Makala haya yamezingatia mikabala ya waandishi wa vitabu vya kiada tofauti kuhusu mtindo wa insha za Kiswahili katika shule za upili. Uchanganuzi wa yaliyomo katika matini za waandishi wa insha za Kiswahili umeonesha mikabala tofauti katika ufundishaji na ujifundishaji wa mtindo wa insha. Uchanganuzi wenyewe uliongozwa na Nadharia ya Mtindo inayoshikilia kuwa mtindo hutegemea mtu binafsi na kila mtu ana mtindo wake. Sehemu kubwa ya data liyokusanywa ilitokana na uchanganuzi wa yaliyomo na hojaji ya wanafunzi na walimu. Machapisho ya waandishi tofauti wa vitabu vya kiada vinavyotumika katika shule za upili nchini Kenya yalichunguzwa. Matokeo ya utafiti yamedhihirisha kwamba, mikabala ya waandishi tofauti imechangia ama kuimarisha matokeo ya mtihani wa kitaifa au kuchangia matokeo duni pia kutegemea uwezo wa kielimu wa wanafunzi wanaohusika. Inapendekezwa kwamba walimu na wanafunzi wanapaswa kupewa uhuru wa kuteua na kutumia vitabu vya kiada tofauti tofauti wavipendavyo na vinavyokidhi mahitaji yao katika kila kidato kulingana na uwezo wao wa kielimu badala ya kuvitegemea vile vilivyonunuliwa na kusambazwa kwa shule na serikali.

## MAREJELEO

Butler, P. (2008). Out of Style: Reanimating Stylistic Study in Composition and Rhetoric. *All USU Press Publications*. 162.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1803

https://digitalcommons.usu.edu/usupress_pubs/162

Corbett, E. (1998). Approaches to the study of style. *Teaching Composition 12(1)*: 83-130.

KIE. (2002). *Kiswahili kwa Sekondari Mwongozo wa Walimu.* Nairobi: KIE.

KNEC. (2020). *Mwongozo wa kusahihishia insha*. Naiobi: Kenya National Examination Council.

KNEC. (2020). *The year 2019 Examination Report*. Nairobi: Kenya National Examination Council.

Milic, L. (1965). *Theories of style and their implications for the teaching of composition and other Essays*. Ilinois: College composition and communication.

Montin, R.A. (2011). *From theory to praxis: Style, dualism, and the composition classroom*. Tasnifu ya Uzamili (MA) isiyochapishwa. Stillwater, OK: Oklahoma State University.

Mumbo, C. & Ngamia, F. (2013). *Johari ya Kiswahili kidato cha pili* Nairobi: East Africa Educational Publishers.

Ngure, A. (2011). *Hazina ya Kiswahili*, kidato cha tatu, Nairobi: Longman Kenya.

Nyariki, E. (2021). Tofauti kati ya muundo na mtindo wa insha. *Taifa Leo*, Februari 22, 2021. Nairobi: Nation Media Group.

Richards, J.C. (2001). *Curriculum Development in Language Teaching*. Cambridge: Cambridge University Press.

Vonyoli A. J, Watuha, A. I, Mutekwa. F.O. ... Waweru, M.K. (2015). *Kiswahili Kitukuzwe: kwa kidato cha tatu, kitabu cha mwanafunzi* (Toleo la tano). Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Vonyoli, A. Watuha, A., Mutekwa, F.O. ... Waweru, M.K. (2014). *Kiswahili Kitukuzwe: kwa kidato cha kwanza, kitabu cha mwanafunzi* (Toleo la tano). Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Vonyoli, A.J, Watuha, A.I, Mutekwa, F.O. ... Waweru, M.K. (2014). *Kiswahili Kitukuzwe*: *kwa kidato cha Nne, kitabu cha mwanafunzi* (Toleo la tano). Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Walibora, K. & Wangendo, F. (2004). *Uhondo wa Kiswahili kwa shule za upili* kitabu cha mwanafunzi kidato 1. Nairobi: Moran (E.A) Publishers.

Wamitila, K.W. & Waihiga, G. (2010). *Chemichemi za Kiswahili* kidato cha pili. Nairobi: Longhorn Publishers.

Wamitila, K.W. (2015). *Chemichemi za Kiswahili* kidato cha nne. Nairobi: Longhorn Publishers.